

Maneno Hayatoshi

Luka 10:25-37 tunakutana na hadithi ya Msamaria Mwema. Kwenye hadithi hii Yesu alitoa changamoto kwamba maneno na mwonekano havitoshi. Ikiwa tunadai kumpenda Mungu, basi tunahitaji kuishi kama yeye.

Hadithi inazungumzia juu ya matu aliyekuwa akisafiri kutoka Jerusalemu kwenda Yeriko. Njiani alivamiwa na majambazi wakampiga na wakamwacha karibu ya kufa pembeni mwa barabara. Alipokuwa amelala pale Kuhani na Mlawi, wanaoitwa 'Watu wa Dini' walimpita bila kumjali. Kwa mshangao akapita, Msamaria, adui aliyechukiwa na kila mtu, akamsaidia mtu huyo kwa kumpa msaada kwa kila alichohitaji. Kwa gharama zake, Msamaria alimpenda na kumjali mtu huyo kwa namna ambayo hakuna mwingine aliyefanya hivyo.

Kuhani na Mlawi wangepahamu maneno mazuri ya kusema, namna ya kuimba kwaya, namna ya kuomba na wamekuwa wakiheshimiwa na watu binafsi ndani ya makanisa yao. Bado ni Msamaria ndiye aliyeonyesha upendo wa Yesu. Dini ya kweli yenya kumpendeza Mungu ni kuishi na kupenda kama Yesu, kuwafikia maskini, wapeke, waliodidimizwa na kuwapenda kwa kila tulichonacho.

Hadithi ilisemwa ikiungwa mkono kwa maneno haya yanayojulikana: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote kwa nguvu zako zote na kwa akili yako yote," na "Lpende jirani yako kama nafsi yako." Yesu alitambulisha mambo haya kama amri zilizo za muhimu sana kwenye Biblia nzima. Kwa nini? Mungu ni Mungu wa upendo na ikiwa imani yetu iko ndani yake kamili ni lazima kuonekane kwa matendo ya upendo na kwa kuwahudumia wengine.

Kwa kawaida kama waamini tunaweza kukamatwa kwa kutunza ile hali ya nje. Tunaweza kusema mambo yaliyo sawa, kwenda kanisani, kuomba na kuabudu lakini matendo yetu na namna tunavyowahudumia wengine itasema hadithi ya tofauti kabisa. Kitabu cha Yakobo 2:14 inauliza swali yafaa nini kama tunasema tunayo imani lakini hatuna matendo ya kuonyesha?

Mungu anataka sisi kuwa watendaji wa imani, kuishi maisha yetu kwa moyo wote kwa ajili ya Yesu na kwa maisha yetu yakiwaelekeza wengine kwake. Ni muhimu kuwa tunatoa maisha yetu kwa mahitaji ya wengine, kuwa kama watumishi ambao tunaweza kuwa tunatembea, kungea mfano wa upendo wa Mungu.

Zingatia!

Kwenye jumuiya yenu kutakuwa na watu kama wasafiri kwenye hadithi na kuhitaji msaada. Unaweza kuchakua kuwapuuza watu hao kama Kuhani na Mlawi walivyofanya, au kuwapenda kama Msamaria. Kwenye eneo lenu mtambue mtu anayeteseka. Anaweza kuwa mgonjwa, mpyeke au wanateseka kujilisha wao wenyewe. Pamoja na marafiki 1 au 2, mweke agano wiki hii kumpenda na kumtumikia mtu huyo.


Omba:

- 1) Mungu atamwonyesha mtu huyo jinsi anavyowapenda.
- 2) Roho Mtakatifu atakuongoza, akikuonyesha jambo la kufanya.



Kikundi cha Uzima kule Chitembo, Zambia walizungukia kijiji chao kuona nani alikuwa akiteseka. Walikutana na bibi wa miaka 72, akiishi mwenyewe bila msaada wowote. Alisema familia yake imeenda kijiji kingine. Hakuwa na chakula. Kikundi cha Uzima kikatafuta familia yake, lakini hawakuweza kuwapata. Hivyo wao wenyewe wakamhudumia, wakamnunulia eneo la kiwanja na kufanya kazi ya kumpania.

- Pilius, Luapula, Zambia



Somo hili limechukuliwa toka "Maneno hayatoshi" limechukuliwa toka "Penda Kijiji Chako".

Kwa maelezo zaidi:

dignityonline.org.uk/publications